MsomiMaktaba.Com

OFISI YA RAISI TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA
ELIMU YA DINI YA KIISLAMU
MTIHANI WA UTAMIRIFU MOCK KIDATO CHA PILI OKTOBA 2020

MUDA:SAA 2:30

**Maelekezo**

1.Mtihani huu una sehemu A,B, na C
2.Jibu maswali yote

SEHEMU A(Alama 20)

1.Katika kipengele (i)-(x) chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kisanduku.

(i) Mapokezi au taarifa ya yale yote aliyoyafanya Mtume (s.a.w) au yaliyotendwa mbele yake na akayaridhia hujulikana kama
A.Hadithi  B Hadithi ya Mtume  C Sunnah  D Sunnah ya Mtume

(ii)Katika elimu ya Hadithi,Matini ina maana ya
A.sehemu ya wasimulizi wa Hadithi  B.mkusanyaji wa Hadithi
C.maneno aliyoyasema Mtume{s.a.w) au maelezo ya swahaba kuhusu mtume
D.maneno yanayohimiza au kukataza kufanya jambo

(iii)Sehemu ya masimulizi ya Hadithi tokea kwa Mtume (s.a.w) au swahaba hadi kuandikwa kwake hujulikana kama
A.Rawi  B.Matini  C Riwaya  D Isnadi

(iv)Sababu kubwa ya funga kufaradhishwa ndani ya mwezi wa Ramadhani ni
A.Shetani hufungwa  B.Watu wengi huacha kufanya maovu
C.Mwezi ulioshuka Qur'an  D.Allah(s.w) ameupa baraka nyingi

(v)Maana halisi ya Faradh 'Ain ni
A.Faradh inayoweza kufanywa kwa uwakilishi
B.Faradhi inayomuhusu kila mtu binafsi isiyo na uwakilishi
C.Faradh muhimu yenye malipo makubwa
D.Faradh kubwa zinazotegemewa katika Uislamu.

(vi) Neno "Sunnah" katika lugha ya kiarabu lina maana ya
A.Mwenendo au mila  B.Jambo la ziada
C.Swala isiyo ya faradh  D.Kitendo cha kujipatia thawabu za ziada

(vii)Katika Qur'an tunafahamishwa kuwa kiigizo chetu waislamu kwa tabia njema ni
A.maswahaba  B.wanazuoni  C.Mtume(s.a.w)  D.Ahl Sunnah

(viii)Katika elimu ya Hadithi neno "Mutafakun alayhi" lina maana gani?
A.Hadithi inapatikana katika kitabu cha Bukhari na Muslim
B.Hadithi inayotumika kutolea Ushahidi
C.Hadithi iliyoandikwa tokea wakati wa mtume (s.a.w)
D.Hadithi iliyoandikwa wakati wa maswahaba.

(ix)Tafsiri ya kwanza na muhimu ya Qur'an ni:
A.Hadithi za mtume(s.a.w)
B.Tafsiri ya Sheikh Abdullah Farsy na maelezo yake.
C.Qur'an yenyewe,sehemu moja hutoa maelezo ya nyingine
D.Maswahaba ambao walikuwepo wakati Qur'an inashushwa

Download More Resources On MsomiMaktaba.Com

MsomiMaktaba.Com

(x) Nini maana ya Umra
A.Kutembelea misikiti katika mwezi wowote na siku yoyote
B.Kutembelea nyumba takatifu ya ka'aba katika mwezi wowote na siku yoyote katika mwaka
C.Kutembelea wagonjwa hospitalini na kuwaombea kila siku
D.Kutembelea yatima na kuwafariji kila mwezi

2.Oanisha maneno kutoka Orodha B na sentensi kutoka orodha A kisha jaza herufi yake katika jedwali

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i)Mfumo wa Maisha unaojinasibisha na kutokuwa na Imani ya dini kabisa.<br>(ii)Kiwango cha mali kinachostahiki kutolewa Zakat<br>(iii)Mfumo wa Maisha ambao wafuasi wake humnasibisha mtume wao kama mwana wa Mungu<br>(iv)Mtume(s.a.w)kuletewa wahy wa kwanza<br>(v)Mfumo au njia ya Maisha anayoifuata mwanadamu katika Maisha yake ya kila siku.<br>(vi)Ujuzi unaoambatana na utendaji<br>(vii)Majina mengine ya Qur'an<br>(viii)Adui mkubwa wa Nabii Adam(a.s) na kizazi chake<br>(ix)Mtu anayemnyenyekea Allah(s.w) kwa kufuata kwa ukamilifu sharia zake zote<br>(x)Chanzo cha fani zote za elimu | A.Qur'an 5:3<br>B.Alhamdu,Ummul Kitaab<br>C.Elimu<br>D.Muislamu<br>E.Daud (a.s)<br>F.Allah (s.w)<br>G.Ukristo<br>H.Qur'an 96:1<br>I.Upagani<br>J.Iblis<br>K.Makkah<br>L..Nisaab<br>M.Muhammad<br>N.Uislamu<br>0.Alfurqaan,Albayaan, Anuur. |

MAJIBU

| Orodha A | i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | | | | | | | | | | |

SEHEMU B(Alama 40)

3.Andika KWELI kama sentensi ni sahihi au SI KWELI ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi

(i)Ushirikina nao ni dini au mfumo wa Maisha unaowaongoza washirikina katika maisha yao ya kila siku……………………………….
(ii)Nguzo za Imani ya kiislamu ni tano…………………………..
(iii)Malaika ni viumbe wasio na matamanio ya kijinsia…………….
(iv)Zaburi ni kitabu alichoteremeshiwa Nabii Issa(a.s)……………………..
(v)Ukristo ni miongoni mwa dini zinazompwekesha Allah……………..
(vi)Katika uislamu hakuna mgawanyo wa elimu ya dini na dunia………………..
(vii)Tawhiid ni elimu inayofundisha kumuabudu Allah kama inavyotakiwa…………….
(viii)Katika lugha ya kiarabu siku ya malipo ni miongoni mwa maana ya dini ………………..
(ix)Uislamu unahimiza kusoma fani za elimu zote isipokuwa uchawi ……………………….
(x)Dini za watu ni mifumo ya Maisha iliyowekwa na wanadamu kwa kuzingatia muongozo wa Allah(s.w)………………………

Download More Resources On MsomiMaktaba.Com

MsomiMaktaba.Com

4.Kwa kutumia maneno uliyopewa,chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi

| |
|---|
| Miraj,Isra,Khadija,Ifraad,Ali bin Abutwalib,Isnad,Qiran,Imam,Yathrib,Zabur,Matini,Qur'an,Abu Jahal,Amina bint Wahhab,Injili,Mtume(s.a.w),Aqaba,Khalifa,masanamu,mwenye nguvu,Abubakar |

A.Swahaba aliyekabidhiwa amana zote za watu alizokuwa nazo mtume (s.a.w)ili azirudishe kwa Wenyewe wakati mtume(s.a.w) anahama kuelekea Madina ni…………………..

B.Miongoni mwa vitabu vya Allah(s.w) alichopewa Nabii Issa(a,s)…………………….

C.Aina ya Hija ambapo Haji anavaa Ihram kwa nia ya kufanya Hija tu bila Umra………….

D.Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake………………………….

E.Kiongozi mwenye tabia njema isiyo na mfano wake katika jamii yake ni………………………………

F.Kiongozi wa mkutano mkubwa katika "Dar-al-Nadwa" wa kumdhuru mtume(s.a.w) kabla ya Kuhamia Madina aliitwa……………………………….

G.Mji wa  Madina kabla ya hijra ya mtume (s.a.w) ulijulikana kama …………………………….

H.Msururu wa wapokezi wa Hadithi……………………………….

I.Mwanamke mjane miongoni mwa matajiri wakubwa wa Makkah aliitwa……………………..

J.Kiongozi wa dola ya kiislamu baada ya kutawafu mtume………………………….

5.Nukuu zifuatazo hazikupangwa katika mtiririko unaotakiwa.Panga nukuu hizo katika mpangilio Sahihi ili kupata maana iliyokamilika.

(a)Historia ya kushuka Qur'an kwa mtume Muhammad (s.a.w) kupitia kwa malaika Jibril (a.s) inasimuliwa vyema na Bibi 'Aisha (r.a) katika hadithi ifuatayo:

A.Basi alikuwa anakwenda Jabar Hira akifanya ibada masiku mengi na alichukua masurufu Kwa ajili hiyo.

B.Kilichoanza katika wahyi wa Mtume(s.a.w) ni ndoto za kweli.

C.Masurufu haya yalipokwisha  alirudi tena kwa Bibi Khadija aliyemtayarishia masurufu kama Yale (ya kwanza) mpaka ikambainikia haki akiwa pangoni Hira.

D.Kisha akaona ni bora kujitenga

E.Alikuwa Mtume(s.a.w) haoti chochote isipokuwa kilitokea kama alivyoota.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

(b)Dalili kwamba binadamu tunahitaji ulinzi wa Mwenyezi Mungu (s.w) dhidi ya shari mbalimbali

A.Nashari ya alivyoviumba

B.Nashari ya hasidi anapohusudu

C.Sema:ninajikinga kwa mola wa ulimwengu wote

D.Nashari la giza la usiku liingiapo

E.Nashari ya wale wanaopilizia (vivia) mafundoni,(wakavunja mashikamano yaliyo baina ya Watu,yaani shari ya mafatani)

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

Download More Resources On MsomiMaktaba.Com

MsomiMaktaba.Com

SEHEMU C(Alama 40)

6.Jibu maswali yote kwa ufupi

(a) (i)Nini maana ya Zakat?..........................................................................................

..............................................................................................................................................

(ii)Bainisha watu aina tano wanaostahili kupewa Zakat? ……………………………..

…………………………………………………………………………………………………………………………………….

(b)Taja aina mbili za Sunnah zinazoambatana na funga ya Ramadhani…………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………..

(c) Taja sharti nne za swala ambazo muislamu anapaswa kuzichunga kabla hajaanza Kuswali

………………………………………………………………………………………………………………………………………

(d) (i) Andika shahada mbili kwa maandishi ya Kiswahili……………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………..

(ii)Andika tafsiri ya shahada mbili kwa lugha ya Kiswahili……………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

(e) Taja nyakati tano zilizoharamishwa kuswali na mtume (s.a.w)………………………………….

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

7. Eleza njia tano za mawasiliano kati ya Allah(s.w) na waja wake……………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………………………

Download More Resources On MsomiMaktaba.Com